**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule 0788400218**

**0754614958**

**M/Mkuu wa Shule 0767303190**

**Matron/Patron 0657158727**

**Shule ya Sekondari KAZIMA**

**S.L.P 369**

**Tarehe 12/04/2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ...............................................................**

**S.L.P .........................**
**...................................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAZIMA HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA MKOA WA TABORA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya .....................

Shule ya Sekondari KAZIMA ipo umbali wa Kilometa 1.5 Mashariki mwa Mji wa Tabora Usafiri kutoka mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Tabora Nauli ni Shilingi 1000/= kwa pikipiki na Shilingi 2000/= kwa bajaji.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe July 2024, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe July 2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31/08/2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni sketi (2) ndefu mpaka kifundo cha mguu, za rangi ya damu mzee na mashati meupe(2) kwa Wasichana na suruali 2 rangi damu ya mzee zenye marinda mawili isiyobana, upana wa chini ni inch 18 – 20 na mashati (2) meupe kwa Wavulana. (vitambaa vya suruali na sketi vyote viwe vya suti vizoto)
ii. Mashati tomato meupe;
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iv. Sare ya Michezo ni sketi(wasichana) fupi ya solo na truck suit damu ya mzee yenye mistari mieupe pembeni, kwenye kola na mikononi isiyo na kofia kwa wasichana na wavulana;
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwawavulana;
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta la damu ya mzee;
ix. Nguo za kushindia gauni (2) za damu ya mzee mshono wa solo na kijuba cha damu ya mzee kwa waislam.
x. Tai ndefu (2) damu ya mzee;
xi. Tisheti (T-shirt) 2 damu ya mzee zenye kola nyeupe na ufito wa damu ya mzee
xii. Raba nyeupe kwa ajili ya michezo.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter books 12
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ;
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator kwa wanafunzi waliochaguliwa tahasusi za HGE, ECA, EGM, PCM, PCB;
vi. Godoro futi $2\frac{1}{2}$ upana
vii. Mashuka Jozi 2 rangi ya blue kwa wavulana na pink kwa wasichana, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1 rangi nyeupe*;*
viii. Nguo za ndani za kutosha;
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 1, jembe 1, toilet brush (brashi ya kusugulia choo) 1, fagio 1 la ndani (softbroom), squeezer 1, hard broom ya ndani 1 na fagio la nje (chelewa) 1.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Michango yote hii ilipwe kwenye akaunti ya shule:

Jina la akaunti: KAZIMA SECONDARY PROJECT ACCOUNT
Account namba: 51001100086 NMB MIHAYO BRANCH

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**


i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**


i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule ELIZABETH N. MASANJA**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** 


**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0788400218**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0767303190**
- **Mwandamizi Taaluma 0756725261**
- **Mwandamizi Malezi 0657158727**

## SHULE YA SEKONDARI YA KAZIMA

## A. FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI ……………………………………….
2. TAREHE YA KUZALIWA ……………………………………………………………
3. MZAZI / MLEZI………………………………………………………….
4. UHUSIANO NA MLEZI ………………………………………………..
5. MAHALI UNAPOISHI MZAZI / MLEZI, MKOA
   …………………….…………
   WILAYA……………………….. MTAA/KIJIJI………………………….
6. MAWASILIANO YA MZAZI / MLEZI…………………………………..
7. KABILA…………………………………………………………………
8. KAZI YA MZAZI/ MLEZI …………………………………………….………
9. WAZAZI WAKO HAI AU WAMEFARIKI WEKA ALAMA YA ( √ )
   - BABA (AMEFARIKI) ( ) BABA YUPO HAI ( )
   - MAMA( AMEFARIKI) ( ) MAMA YUPO HAI ( )
10. NDUGU WENGINE WA KARIBU NA MZAZI / MLEZI AMBAO WANAWEZA KUTUMIKA KAMA WALEZI WA WANAFUNZI KAMA MZAZI / MLEZI HUSIKA HAYUPO

| | JINA | MAHALI | NAMBA ZA SIMU |
|---|---|---|---|
| a) | …………………………. | …………………….. | ……………………. |
| b) | ………………………….. | ……………………… | ……………………. |
| c) | ………………………….. | ……………………… | ……………………. |
| d) | ………………………….. | ……………………… | ……………………. |

## B. MAKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi ( jina la mwanafunzi) ……………………………………………….. nimesoma na kuelewa sheria, kanuni za taratibu za shule ya bweni, niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapo kuwa shule adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

……………………………………… ……………………………..
Saini ya Mwanafunzi Saini ya Mkuu wa shule

MINISTRY OF EDUCATION SCIENCE AND TECHNOLOGY

KAZIMA SECONDARY SCHOOL

P.O.BOX 369

**TABORA**

……………………

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION.**

This form must be completed by a government medical officer

Student's full name ……………………………………………………………………………….

Present age ……………………………………………………………………………………….

Blood test …………………………………………………………………………………………

School examination ……………………………………………………………………………

T.B test ……………………………………………………………………………………………

Asthma ……………………………………………………………………………………………

Eye disorder ………………………………………………………………………………………

Nose disorder ……………………………………………………………………………………..

Ear disorder ………………………………………………………………………………………

Skin disease……………………………………………………………………………………….

Anaemia ………………………………………………………………………………………….

Chest ……………………………………………………………………………………………...

Operations ………………………………………………………………………………………..

Serious accidents ……………………………………………………………………………..

Any other infections disease ……………………………………………………………………..

Pregnancy ………………………………………………………………………………………..

Additional information e.g. physical defects or impairment, chronic or family diseases etc

…………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………

I certify that I have personally examined Mr./miss ………………………………………………………and found him/her fit unit to purpose studies

Signature………………………………………………..

Designation……………………………………………..

(Official rubber stamps) ……………………………….………………………